

## **Dhambi-Kuitupilia Mbali**

Unaweza kufikiria uhusiano wako na muumba wako ambapo unaweza "kutembea na kuongea naye kama marafiki pete na kidole." Unashikana mikono na sauti zinaungana kwa kuangua kicheko? Adamu alikuwa na hali hiyo. Alimfahamu vizuri Mungu hata kufikia hatua ya kujua hata sauti ya Mungu alipokuwa akitembea bustanini, Mwanzo 3:8. Lakini Adamu aliacha yote kwa ajili ya kipande cha tunda lililokatazwa.

Tunaweza kujifunza nini kutokana na hali hii?

"Ukomboeni wakati." Wakristo wanatakiwa kujifunza kujitahidi kwa kadri wavezavyo katika kila fursa. Hata ingawa tunafahamu kuwa uhai ni kama mvuke (Yakobo 4:14). Bado tunashikwa na mazoea ya kudhani kuwa tuna muda mwingi hapa duniani. Hivyo yanayotakiwa kusemwa tunayaacha bila kuyasema. Kinachotakiwa kufanywa tunakiacha bila kukifanya na bila kuukomboa wakati na kutusababishia tu matatizo mengi. Na sasa, sisi sote, pengine tungependa tupate fursa ya angalau kumkumbatia mtu fulani kwa mara ya mwisho tu. Au angalau kumwambia maneno ya mwisho mtu anayefariki. Kufumba na kufumbua Adamu alijikuta ameharibu uhusiano wake na Baba. Na hakuwa na lakufanya ili iwe ajuwa, kufanya upatanisho wa kile ambacho ameshakiharibu. Kama ambavyo hatuwezi kuahirisha kutuma ujumbe mfupi wa simu au barua pepe pale tunakuwa tunakisoma tulichokituma, eti?? Hivyo, kupitia makosa ya Adamu tujifunze jinsi ya kufanya maamuzi ya busara. Maamuzi mabovu yanayotujutisha sasa tuliyowahi kufanya si yanatosha?

"Huwezi kumlamu mtu." Kama ungeweza kuuona uso wa Mungu, unadhani ilikuwaje Adamu alipojaribu "kukwepa makosa" "sawa,ni wewe uliyenipa huyu mke." Twaishi katika utamaduni wa kuepa majukumu. "nilizaliwa hivi hivi" "nimeumbwa hivi hivi" "Utoto wangu ulikuwa mgumu." "Marafiki zangu walinifanya nifanye hili". Linapokuja suala la dhambi, kwa Mungu hakuna kukwepa shutuma. Hakuna jaribu linalozidi uwezo wetu wa kulipinga (1 Wakorintho 10:13). Ni kweli tunaweza kumpinga Ibilisi, naye atatukimbia, Yakobo 4:7. "kurusha mpira" haitasadida kwa Mungu. Kwa kuwa tunafahamu, na kwa sababu hiyo "natumtii Mungu" Yakobo 4:7

"Tunamhitaji mwokozi" Hivi unaweza kujua hisia alizokuwa nazo Adamu maisha yake yote? Maumivu ya kudumu, hatia ya kudumu inayotokana na kujua alilolifanya. Miiba na michongoma, ardhii ngumu, vivu, uuaji, chuki; vyote vilizaliwa kwa sababu ya uamuzi? Na kisha, hakuwa na chakufanya ili kutatua tatizo alilosababisha mwenyewe. Ndiyo, Mungu aliwapa dhabihu za wanyama, lakini zilikuwa ni kumbukumbu za walichofanya. Alichohitaji Adamu ili kuondoa hatia ya dhambi na maumivu, tunacho leo katika Yesu Kristo. Ingawaje Mungu alitabiri ujio wa Yesu katika Mwanzo 3:15, Adamu hakuwahi kuonja raha ya kuwa ndani ya Kristo. Nasi leo tumevunja uhusiano baina yetu na Baba kutokana na dhambi. Matumaini yetu yanaweza kueleweka katika yeche! Mungu alifanya hatua ya kwanza; akamtuma mwanawele ili kuweka mambo sawa. Na sasa, hebu nasi sote na tuone haja ya kumgeukia Kristo! Na tusiyatupilie mbali maisha yetu!